



JARIDA MAALUM

Toleo la 21 | MEI, 2021

OFISI YA WAZIRI MKUU



MAJALIWA: WATANZANIA TUTOE USHIRIKIANO WAKATI WA SENSA

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ametoa wito kwa watanzania kutoa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha utekelezaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi litakalofanyika Agosti 28, 2022.

NDANI...

WAZIRI MKUU AKABIDHI MAGARI 184 KWA HALMASHAURI NCHINI

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amekabidhi jumla ya magari 184 kwa maafisa elimu msingi wa Halmashauri ikiwa ni mkakati wa Serikali ya awamu ya sita ya kuendelea kuboresha sekta ya elimu nchini.



Ofisi ya Waziri Mkuu



owm_tz



www.pmo.go.tz

JARIDA LA MTANDAONI



MAJALIWA: WATANZANIA TUTOE USHIRIKIANO WAKATI WA SENA

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ametoa wito kwa watanzania kutoa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha utekelezaji wa zoezi la Sena ya Watu na Makazi litakalofanyika Agosti 28, 2022.

Amesema takwimu zitakazopatikana katika zoezi hilo zitatumiwa na Serikali katika utungaji, ufuatiliaji na uboreshaji wa sera mbalimbali pamoja na kufanya maamuzi kwa kuzingatia vigezo vya kitakwimu.

Ametoa wito huo Mei 22, 2021 wakati wa uzinduzi wa kitabu cha mkakati wa usimamizi na utekelezaji wa Sena ya watu na makazi ya Mwaka 2022, katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu Jijini Dodoma.

“Ni dhahiri kuwa, takwimu rasmi zitaiwezesha Serikali ya Awamu ya Sita na wadau wengine kufuatilia na kutathmini Malengo yaliyofikiwa katika kutekeleza Mipango ya Maendeleo iliyokusudiwa kwa lengo la kukuza uchumi na kupunguza umaskini na hatimae kufikia Dira yenyewe”.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Hemed Suleiman Abdulla amesema kuwa watatoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha zoezi hili linafanyika kwa mafanikio.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhandisi Hamadi Masauni amesema kuwa watahakikisha sena ya watu na makazi kwa mwaka 2022 inafanyika kwa ufanisi mkubwa kwa kutambua umuhimu wa sena kwa maendeleo ya nchi yetu.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dkt. Albina Chuwa amesema Kuwa Sena ya Mwaka 2022 inakwenda kutoa taarifa za kitakwimu kwenye ngazi ya kitongoji tofauti na sena za miaka ya nyuma ambazo zilikuwa zinaishia katika ngazi ya vijiji.

Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar Mayasa Mwinyi amesema kuwa Sena ya mwaka 2022 itakuwa ya kipekee na bora kutokana na matumizi ya teknolojia yatakayowezesha kupunguza kazi, matokeo kutolewa ndani ya muda mfupi na gharama za uendeshaji pia zitapungua



WAZIRI MKUU AKABIDHI MAGARI 184 KWA HALMASHAURI NCHINI.

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amekabidhi jumla ya magari 184 kwa maafisa elimu msingi wa Halmashauri ikiwa ni mkakati wa Serikali ya awamu ya sita ya kuendelea kuboresha sekta ya elimu nchini.

Amesema kuwa Serikali itaendelea kusimamia mchakato wa ununuzi wa magari 184 yatakayogawiwa kwa maafisa elimu Sekondari.

Hafla hiyo imefanyika (Mei 21, 2021) katika viwanja vya Shule ya Sekondari Kibasila, Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika tukio hilo, Waziri Mkuu amezitaka Halmashauri zilizopokea magari zizingatie taratibu za serikali katika matumizi na matengenezo ya magari hayo.

“Magari haya mmekabidhiwa, maafisa elimu na wakurugenzi wa Halmashauri, tukute gari limepaki kisa limekosa ‘Service’ utakuwa umekosa kazi, lazima tuambizane ukweli, magari haya lazima

yafanye kazi kwa zaidi ya miaka mitano hadi sita”

Amesema kuwa magari hayo ni kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwa Maafisa Elimu, na yametolewa na Serikali ili yasaidie kuharakisha shughuli za utekelezaji wa majukumu katika sekta ya elimu.

Aidha, Waziri Mkuu amewataka Wakuu wa Mikoa na Makatibu tawala wa mikoa kuchukua hatua ikiwa magari hayo yatatumika tofauti na malengo yaliyotarajiwa “hakikisheni magari haya yanakwenda kutekeleza shughuli za elimu kwenye halmashauri zenu na si vinginevyo”

Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Ummu Mwalimu amesema Magari hayo yamenunuliwa na Serikali kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (EP4R) kwa gharama ya shilingi bilioni 16.4.

Amesema kuwa hii ni awamu ya pili ya ununuzi wa magari baada ya awamu ya kwanza ambayo magari 26 yalinunuliwa kwa ajili ya usimamizi wa elimu katika ngazi ya Mikoa.





Muonekano wa baadhi ya magari 184 yametolewa na serikali kwa Maafisa Elimu katika Halmashauri zote nchini ili yasaidie kuharakisha shughuli za utekelezaji wa majukumu katika sekta ya Elimu, magari hayo yamekabidhiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa leo Mei 21, 2021 kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari ya Kibasila jijini Dar es Salaam



MAJALIWA: TUMIENI URITHI WA UKOMBOZI KUJIKOMBOA KIUCHUMI

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ameitaka jamii kuutumia urithi wa ukombozi uliopo nchini kujikomboa kiuchumi na kifikra.

Amesema kuwa ni vyema jamii ambazo zinatumia au zina miliki maeneo au miundombinu ya urithi wa ukombozi wa Afrika ikavitunza na kupata ushauri wa kitaalamu wa kuanzisha makumbusho na kuvutia utalii katika eneo hilo ili kujiongezea kipato.

Ametoa kauli hiyo (Ijumaa, Mei 21, 2021) wakati wa Ufunguzi wa Kongamano la kutambua na kuenzi mchango anuai wa historia ya Tanzania katika Ukombozi wa bara la Afrika na Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni na Michezo, kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.

“Nimeambiwa yapo maeneo zaidi ya 225 ya urithi wa ukombozi nchini, maeneo hayo ni fursa kwetu iwapo tutayatumia vyema. Urithi huu wa ukombozi ukiondoka umeondoka, haurudi mara ya pili.

Hivyo, ni matarajio yangu kuwa mikoa ya Lindi, Ruvuma (Songea), Mtwara na Mbeya itakuwa mikoa ya kwanza kunufaika na zao jipya hili la utalii wa kiukombozi”

Aidha, Waziri Mkuu amesisitiza kuwa jukumu la kuhifadhi na kulinda urithi wa ukombozi tulionao ni la kila mmoja ili vizazi vijavyo viweze kujifunza na kuendeleza.

Amesema kuwa makundi yote au mtu yoyote ambaye ana mali za urithi wa ukombozi aviwasilishe katika Makumbusho ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika iliyopo Dar es Salaam ili vihifadhiwe kitaalamu visije vikapotea

Naye, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Innocent Bashungwa amesema kuwa lengo la kongamano hilo ni kuelimisha umma umuhimu wa kujikomboa kiuchumi na kifikra kupitia uhifadhi na utangazaji wa zao la utalii wa kiukombozi.



MAJALIWA: WAHARIRI ZINGATIENI VIWANGO NA UBORA KATIKA UANDISHI.

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka wahariri wa vyombo vya habari wahakikishe wanazingatia weledi na maadili katika uandishi wa habari ili umma uweze kupata habari zenye ubora.

Ametoa wito huo Mei 20, 2021 wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 10 wa Jukwaa la Wahariri na kongamano la kitaaluma, Mkoani Morogoro

Amesema kuwa utendaji unaozingatia weledi ni chachu ya kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na wamiliki wake.

“kaulimbiu yenu ya Vyombo vya Habari na Maendeleo inahamasisha uandishi wa uwajibikaji. Vyombo vya habari vinapaswa kutambua katika kila habari vinayoiandika kuwa nyuma yake kuna masilahi ya taifa. Visipofanya hivyo, upotoshaji unaweza kuigawa nchi yetu, kuhatarisha amani na mshikamano wetu”.

Aidha Waziri Mkuu ameviasa vyombo vyote vya habari nchini kuhakikisha vinatanguliza Uzalendo, Utaifa na Maslai ya Nchi katika kufanya kazi “Mjenga Nchi ni Mwananchi. Hakuna mwingine zaidi yenu wa kulisemea Taifa letu”

Naye, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa amesema kuwa kupitia Wizara ninayoiongoza imeendelea kushirikiana vema na vyombo vya habari ili kuviwezesha vyombo hivyo pamoja na waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao bila vikwazo huku wakizingatia Sheria, Kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari.

Kwa upande wake Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania Deodatus Balile amesema jukwaa hilo litaendelea kushirikiana na Serikali na amepongeza dhamira ya Serikali ya awamu ya sita ya kuyaishi maono yake ya kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari.



KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S.L.P 980
40480 Dodoma,
Baruapepe: ps@pmo.go.tz, Simu:+255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz